# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.

Sheria za majimbo **fulani** zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu **vituo ya ukaguzi** na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## KAMA UNA ULIZWA KUHUSU HALI YAKO YA UHAMIAJI

- Uko na haki ya kubakiya kimya.
- Usiongeye juu ya  hali yako ya uhamiaji ao ya uraia na polisi ao maafisa wa uhamiaji.
- Huna haja ya kujibiya maswali kuhusu fasi kwenye ulizaliwaka, kama weye uko raia wa Marekani, ao namuna uliingiaka mu inchi. (Sheria tofauti zinatumika ku mipaka ya kimataifa na viwanja ya ndege, na pia ku watu wenye wako na aina fulani za viza za watu wenye hawako wahamiaji, ikiwa amo watalii na wasafiri wa biashara.)
- Kama uko na miaka zaidi ya 18, kumbuka kubeba vitambulisho yako ya uhamiaji kila wakati. Kama hauna barua za uhamiaji, sema: “Sipendi kujibiya maswali yenu.”
- Usiseme bongo kuhusu hali yako ya uraia ao kupana barua za bongo.



